Jarida La MELI

TOLEO LA 7 APRILI – JUNI 2023

MSCL KUONGEZA WIGO WA AJIRA..

UK. 2

Serikali kutumia Bilioni 100..

UK. 4

MSCL YAWATUNUKU WATUMISHI 11...

UK. 9

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan akitoa maelekezo kwa MSCL na makandarasi juu ya kuzingatia ubora na vigezo katika umaliziaji wa ujenzi wa meli mpya ya MV. Mwanza Hapa Kazi Tu wakati alipoingia ndani ya meli hiyo kukagua maendeleo ya ujenzi wake. (Picha na Edmond Rutajama)

RAIS SAMIA AAHIDI KUPANDA MV. MWANZA

Na. Shani Chogelo

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Samia Suluhu Hassan ameahidi kuwa wa kwanza kuipanda Meli mpya ya MV. Mwanza Hapa Kazi Tu mara tu ujenzi wa meli hiyo utakapokamilika.

Aliyasema hayo Juni 14, 2023 wakati akizungumza na wananchi wa Mkoa wa Mwanza katika Bandari ya Mwanza kusini alipofanya ziara ya ukaguzi wa mradi wa ujenzi wa meli hiyo unaotekelezwa na Kampuni ya Huduma za Meli (MSCL) chini ya Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi.

Aidha, Rais Samia ameipongeza MSCL kwa usimamizi mzuri wa ujenzi wa meli hiyo ambayo imefikia asilimia 85 na hivyo kuelekeza kuendelea kuisimamia ili ikamilike kwa wakati na kwa kuzingatia viwango vinavyotakiwa kimataifa.

"Niwashukuru sana mainjinia walioko hapa na wafanyakazi waliopo hapa, wakandarasi waliopo nawashukuru sana kazi zinakwenda vizuri, meli inakwenda kubeba abiria wengi 1,200 na tani 400 na hii ndio maana tuliyosema tunakwenda kuifungua Tanzania kiuchumi, kuwa na miundombinu ni jambo moja lakini kwa sisi watanzania kufanya kazi kwa bidii tukazalisha mashambani na viwandani ili bidhaa zetu zisafirishwe kwenda nchi jirani ndio jambo la pili na ndio jambo kubwa," Alisema.

"Nimeambiwa kuwa meli hii ndani ya kipindi kifupi itakuwa tayari, nataka niwaahidi ikiwa tayari nitakuwa wa kwanza kuja kupanda humu, nitaifungua mwenyewe nikiongozana nanyi wanamwanza tuingie humu tuzungushwe mpaka eneo fulani, kwasababu baada ya siku hiyo sidhani kama tutakuja kuipanda tena sisi wengine," Alieleza.

Kwa upande wake Mkurugenzi Mtendaji wa MSCL Ndg. Eric Hamissi wakati akitoa taarifa ya ujenzi wa meli ya MV. Mwanza hapa Kazi Tu

Inaendelea Ukurasa wa 2..

Mabaharia wa MSCL wakiwa katika picha ya pamoja wakati wa maadhimisho ya siku ya Mabaharia duniani yaliyofanyika viwanja vya furahisha jijini Mwanza. (picha na Shani Chogelo)

MSCL KUONGEZA WIGO WA AJIRA ZA UBAHARIA SERIKALINI

Na. Shani Chogelo

Mkuu wa Wilaya ya Ilemela Mhe. Hassan Masala ameishukuru Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Rais Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuendelea kutenga fedha kwa ajili ya kujenga meli mpya ya abiria na mizigo ya MV. Mwanza Hapa kazi Tu pamoja na ukarabati wa meli ya MV. Umoja.

Mhe. Masala amesema kuwa miradi hiyo inayoendelea pamoja na miradi inayotarajiwa kutekelezwa ni ongezeko la fursa za ajira za mabaharia serikalini kupitia Kampuni ya Huduma za Meli.

"Kuendelea na ujenzi wa meli mpya ya abiria na mizigo ya MV. Mwanza Hapa kazi Tu na ukarabati wa MV. Umoja utakapokamilika utaongeza nafasi za ajira kwa mabaharia na kutoa fursa ya kipekee kwa vijana ikiwemo jinsia ya kike kujiunga kwa wingi kwani fani hii bado imetawaliwa Zaidi na wanaume kuliko wanawake," Alisema.

Alisema hayo wakati wa kilele cha maadhimisho ya Siku ya Mabaharia Duniani yaliyofanyika katika Viwanja vya Furahisha, Wilaya ya Ilemela, Mkoani Mwanza.

Akiongea kwa niaba ya mabaharia walioshiriki maonesho hayo Nahodha Bravius Byarugaba wa MSCL alisema kuwa ongezeko la meli kupitia miradi mbalimbali inayoendelea kutekelezwa na Serikali kupitia MSCL itakuwa mkombozi mkubwa kwa kada ya ubaharia Tanzania.

"Maadhimisho hayo ya siku ya mabaharia kufanyika katika mkoa wa Mwanza yamekuwa ni fursa nzuri kwa Kampuni ya MSCL kujitangaza lakini pia yamekuja na elimu ya kutunza na kulinda mazingira hasa-hasa vyanzo vya maji".

Hata hivyo, akizungumza wakati wa kufungua maonesho hayo Waziri wa Uchumi wa Bluu na Uvuvi Zanzibar Mhe. Suleiman Masoud Makame alisema kuwa Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mhe. Dkt Samia pamoja na Serikali ya awamu ya nane inayoongozwa na Mhe. Dkt. Hussein Mwinyi zimeweka kipaumbele kuwekeza katika miundombinu na vyombo vya usafiri kwa njia ya maji kama vile ukarabati, ujenzi na ununuzi wa meli mpya ambazo zitasaidia katika kuongeza ajira za mabaharia na kukuza uchumi wa nchi.

"Kazi ya Ubaharia sio uhuni kama wengi wanavyoichukulia, hii ni kada yenye weledi wa kutosha na wataalamu mahiri ambao wana taaluma na wamekuwa na mchango mkubwa katika kukuza uchumi wa nchi na Dunia kwa asilimia zaidi ya 80 katika sekta ya usafiri kwa njia ya maji".

Maadhimisho ya maonesho ya siku ya Mabaharia Duniani huwakutanisha mabaharia na wadau wa sekta ya usafiri kwa njia ya maji na kwa mwaka 2023 yalibeba kauli mbiu isemayo "Miaka 50 ya MARPOL uwajibikaji wetu unaendelea".

RAIS SAMIA AAHIDI KUPANDA MV. MWANZA ....

InatokaUkurasa wa 1..

alimshukuru Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuendelea kutoa pesa za kukamilisha mradi huo na kuahidi kuiendesha meli hiyo kwa manufaa pindi itakapokamilika.

Mmoja wa wananchi waliohudhuria ziara hiyo jijini Mwanza, Bi. Celina Joseph aliishukuru Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mhe. Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuendeleza miradi hiyo ambayo wananchi wengi walikuwa na dhana ya kuwa ingeendelea kusuasua.

"Kukamilika kwa mradi huu kutakua na manufaa sana kwa wakazi wa kanda ya ziwa na kuifanya Mwanza kua kitovu cha usafirishaji na kukuza mzunguko wa fedha utakaofungua uchumi sio tu kwa kanda ya ziwa bali hata nchi jirani za Kenya na Uganda."

Meli ya MV.Mwanza Hapa Kazi Tu itakapokamilika itakuwa ni meli kubwa ya kwanza ya abiria na mizigo kujengwa katika ukanda huu wa Afrika Mashariki yenye uwezo wa kubeba abiria 1200 na tani 400 za mizigo na inatarajia kuanza safari zake mwisho wa mwaka huu 2023.

WANANCHI WAISHAURI MSCL KUTOA HUDUMA BAHARINI

Na. Kelvin Mmanda

“Nashauri MSCL mpanue wigo wa shughuli zenu nje ya nchi hasa huku bahari ya hindi, kwa sasa dunia imepanuka na kuna wafanyabiashara wengi ambao wanataka kusafirisha bidhaa zao kwenda nje ya nchi ama kuleta nchini, hivyo ni vyema mkafikiria kuwa na meli huku bahari-ni,’’ Ndg. George Agusti-no mmoja wa wateja walio-tembelea banda la Kampuni ya Huduma za Meli katika Maonesho ya 47 ya Kimataifa ya Biashara maaru-fu SabaSaba alishauri.

Afisa Utekelezaji Mwandamizi wa MSCL, Bw. Baraka Bigambo (kushoto) na nahodha wa Kampuni (kulia) Bw. Juma Mtangi wakitoa elimu kuhusu huduma zinazotolewa na MSCL na Fursa zinazopatikana kwenye usafiri wa njia ya maji. (Picha na Kelvin Mmanda)

Vile vile Ndg. Deogratias Yesaya alishauri kuwa uwepo wa meli ya MSCL inayosafirisha mizigo kutoka nje ya nchi kuja nchini kupitia bahari kutaleta chachu ya kuungana kwa Taasisi za Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari nchini (TPA) na Shirika la Reli nchini TRC na hatimaye kuwepo na ufanisi wa usafirishaji wa mizigo kutoka nje hadi nchi zinazopakana na maziwa makuu

“Kama MSCL itaamua kuwa na meli huku baharini itawarahisishia wafa-nyabiashara kutoka nchi za Burundi, DRC na Uganda na hata Malawi kusafirisha mizigo yao kwa haraka wakiamini kuwa kutaku-wa na ushirikiano baina ya Bandari ya Dar es Salaam na hatimaye kubebwa na mabehewa na kisha meli za MSCL hadi nchini mwao kupitia Ziwa Victoria, Tanganyika na Nyasa,” Alifafanua.

Akizungumza baada ya kuwa-hudumia wateja katika maonesho hayo, Afisa Utekelezaji Mwandam-izi Ndg. Baraka Bigambo alisema kuwa wadau wengi walijitokeza kupata uelewa kuhusu huduma zinazotolewa na MSCL na kukiri kupokea ushauri waliopewa na kuufanyia kazi.

“Tumepokea Wananchi, wafanyabiashara na wasafirishaji kwenye banda letu, tumepokea ushauri zaidi ya 20 wakizungum-zia maboresho mbalimbali lakini wengi walikuwa wamejikita kuitaka MSCL ihamishie huduma zake bahari ya Hindi, nasema tumey-apokea maoni hayo na kuahidi kuyafanyia kazi kwani bado Serikali ina azma ya kutekeleza hilo,” alieleza.

Maonesho hayo yanayofanyika kila mwaka Kitaifa Jijini Dar Es Salaam yalifunguliwa rasmi tarehe 28.06.2023 na Waziri Mkuu Mhe. Kassim Majaliwa na kuhitimishwa na Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mhe Dkt Hussein Ally Mwinyi.

Mkuu wa Wilaya ya Kigamboni Mhe. Halima Bulembo (wa pili toka kulia) akiwa katika picha ya pamoja na watumishi wa Kampuni ya Huduma za Meli (MSCL) wakati alipotembelea banda hilo katika maonesho ya Sabasaba Jijini Dar es Salaam. (Picha na Kelvin Mmanda)

Serikali kutumia Bilioni 100 kuimarisha Uchukuzi kwenye Maziwa Makuu 2023/24

Na. Abdulrahman Salim

Tanzania ni miongoni mwa nchi chache barani Afrika zilizobahatika kuzungukwa na maji kwa asilimia Zaidi ya 6 ikijumuishwa maziwa makuu; Victoria, Tanganyika na Nyasa pamoja na bahari ya Hindi.

Kuzungukwa na maziwa haya makuu ni fursa ya kipekee katika kuzihudumia nchi ambazo hazina milango ya bahari kama vile Uganda kwa Ziwa Victoria, Burundi, Zambia, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Watu wa Kongo (DRC) kwa Ziwa Tanganyika na Malawi kwa Ziwa Nyasa.

Usafiri kwa njia ya maji inasemekana kuwa ni usafiri wa gharama nafuu Zaidi duniani kwasababu meli ina uwezo wa kubeba mizigo mikubwa na mingi kwa pamoja jambo ambalo hupunguza tozo za mizigo kuliko aina nyingine za usafiri ikiwemo wa ardhini kama vile malori na treni pamoja na hata usafiri wa angani. Njia ya maji inaaminika kuwa na gharama nafuu ya matengenezo tofauti na barabara na hivyo kutokuwa na kodi katika matumizi yake.

Hata hivyo, Serikali ya Awamu ya Sita chini ya Uongozi wa Rais Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan imedhamiria kuimarisha usafiri na usafirishaji wa abiria na mizigo katika maziwa makuu kupitia Kampuni ya Huduma za Meli (MSCL) chini ya Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi ambayo imetenga kiasi cha Shilingi bilioni 100 kwa mwaka wa fedha 2023/2024 kama muendelezo wa kufikia azma hiyo.

Akiongea wakati wa uwasilishaji wa bajeti hiyo tarehe 19.05.2023 Bungeni Jijini Dodoma, Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi Mhe. Prof. Makame Mbarawa alisema kuwa kwa mwaka wa fedha 2023/2024 Serikali kupitia Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi imeitengea MSCL kiasi cha Shilingi Bilioni 100 kwa ajili ya kutekeleza miradi mbalimbali.

"Serikali kupitia MSCL ipo katika hatua za mwisho za majadiliano na Mkandarasi ili kuwezesha kuanza ujenzi wa meli mpya tatu (3) pamoja na kiwanda cha kujenga meli kitakachojengwa Ziwa Tanganyika. Kati ya meli hizo mbili (2) ambazo ni: Meli ya mizigo yenye uwezo wa kubeba tani 3,500 na Meli ya abiria na mizigo yenye uwezo wa kubeba abiria 600 na tani 400 za mizigo zitajengwa katika Ziwa Tanganyika; Meli moja (1) ya mizigo yenye uwezo wa kubeba tani 3,000 za mabehewa ya mizigo itajengwa katika Ziwa Victoria."

Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi wa Kampuni ya Huduma za Meli (MSCL) Mej. Jen. Mst. John Mbungo (kulia) pamoja na Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya Huduma za Meli (MSCL) Ndg. Eric Hamissi akisalimiana na Injinia Prisca Mniko nje ya Viwanja vya Bunge Jijini Dodoma muda mfupi kabla ya kuingia Bungeni.

Pamoja na hayo katika kuendelea kurejesha na kuongeza huduma za kufufua na kukarabati meli zilizosimama kutokana na uchakavu Serikali kwa mwaka wa fedha 2023/2024 ina mpango wa kukarabati meli ya kubeba mafuta ya MT.Nyangumi na ukarabati wa meli ya MT.Ukerewe kwa Ziwa Victoria.

Kwa upande wa Ziwa Tanganyika Serikali ina mpango wa kujenga kiwanda cha kujengea meli, Ukarabati wa MV.Liemba, ukarabati wa boti ya mwendokasi (Sea Worriors), Ujenzi wa meli mpya ya mafuta, kufanya ukaguzi wa kina wa meli ya MV.Mwongozo Pamoja na kutafiti aina ya ujenzi wa meli ya Mizigo katika bahari ya Hindi.

Aidha miradi inayoendelea katika Ziwa Tanganyika ni pamoja na ukarabati wa meli ya mafuta ya MT Sangara ambayo hadi sasa imefikia asilimia 92, ukarabati wa MV Liemba upo katika hatua ya kumpata mzabuni wa ukarabati, meli ya MV Mwongozo ipo katika hatua za kumpata Mhandisi Mshauri ili kufanya tathmini ya kina na kuishauri Serikali kuhusu ukarabati wa meli hiyo.

Kwa Ziwa Victoria miradi inayoendelea kutekelezwa ni pamoja na ujenzi wa MV.Mwanza Hapa Kazi tu ambayo imefikia asilimia 85 ikitarajiwa kukamilika mwishoni mwa mwaka 2023, Ukarabati wa meli ya mizigo ya MV.Umoja ambao nao umefikia asilimia 95 ikisubiri kukamilika mapema mwezi Augosti 2023.

Bodi na Menejimenti ya Kampuni ya Huduma za Meli inaahidi kushirikiana vyema na Rais Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan kuhakikisha kuwa malengo hayo yanatimia kwani ukamilifu wa miradi hiyo ni fursa ya kuongeza mapato ya Serikali kupitia kusafirisha mizigo katika maziwa makuu hali itakayopelekea kukuza biashara baina ya nchi za Afrika Mashariki na kati.

Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi wa Kampuni ya Huduma za Meli (MSCL) Mej. Jen. Mst. John Mbungo (wa pili toka kushoto) akiwa Bungeni kufuatilia Bajeti ya Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi iliyokuwa inawasilishwa tarehe 22.05.2023.

HABARI PICHA

Wajumbe wa Bodi ya Wakurugenzi ya MSCL Balozi. Prof. Costa Ricky Mahalu (kushoto) na Nahodha Ibrahim Bendera (katikati) wakimsikiliza Mkurugenzi wa Huduma za Meli na Utaratibu wa Shughuli za Bandari TPA Nahodha Yusuph Mwingamno ambaye pia ni Mjumbe wa Bodi ya MSCL akifafanua namna meli inavyofanya kazi katika Ziwa Nyasa.

Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi Mhe. Prof. Makame Mbarawa (kulia) akiongea na Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi wa Kampuni ya Huduma za Meli (MSCL) Mej. Jen. Mst. John Mbungo (wa pili toka kushoto) pamoja na Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya Huduma za Meli (MSCL) Ndg. Eric Hamissi muda mfupi kabla ya kuwasili kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan katika Bandari ya Mwanza Kusini, Jijini Mwanza.

Kaimu Balozi wa Tanzania nchini Burundi Mhe. Joachim Nyingo (wa tatu toka kushoto) akiwa katika picha ya pamoja na Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya Huduma za Meli Ndg. Eric Hamissi (wa pili toka kushoto) pamoja na wadau wa sekta ya uchukuzi wa nchi za Burundi na DRC nje ya jengo la Ubalozi wa Tanzania nchini Burundi

Mabaharia wakiwa katika mavazi ya uokoaji wakati wakitoa elimu kwa wadau na wananchi waliotembelea katika banda la Kampuni ya Huduma za Meli (MSCL) katika Viwanja vya Furahisha Jijini Mwanza (Picha na Shani Chogelo)

Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi wa Kampuni ya Huduma za Meli (MSCL) Mej. Jen. Mst. John Mbungo (kulia waliokaa) pamoja na Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi wa Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania (TPA) Balozi Ernest Mangu (kushoto waliokaa) tarehe 28.06.2023 wakisaini maridhiano ya mapendekezo ya timu ya wataalamu kutoka taasisi hizo mbili kurejesha mali na miundombinu wezeshi kibiashara ya MSCL iliyokuwa imehamishiwa TPA kwa sheria ya Bandari ya Mwaka 2004 ikiwa ni utekelezaji wa agizo la Serikali.

TUFUATE KWENYE MITANDAO YETU YA KIJAMII

mscltz **Meli TV**

Baadhi ya Wajumbe wa Bodi ya Wakurugenzi Benki Kuu ya Tanzania (BOT) wakiwa na Menejimenti ya Benki hiyo Tawi la Mwanza pamoja na Menejimenti ya MSCL walipotembelea eneo la injini ya meli kwa ajili ya kupatiwa maelezo juu ya namna meli ya MV Mwanza Hapa kazi Tu itakavyofanya kazi mara tu baada ya meli hiyo kukamilika

BODI YA BOT WARIDHISHWA MAENDELEO YA MRADI WA MV. MWANZA.

Bodi ya Wakurugenzi ya Benki Kuu ya Tanzania (BOT) ikiongozwa na Naibu Gavana uthibiti na usimamizi wa sekta ya fedha wa Benki ya Tanzania (BOT) Bi. Sauda Kassim Msemo, wameridhishwa na maendeleo ya mradi wa ujenzi wa meli ya MV. Mwanza iliyoko bandari ya Mwanza Kusini jijini Mwanza.

Akizungumza kwa niaba ya Mwenyekiti wa Bodi hiyo Bi. Sauda alisema kuwa Bodi hiyo imeridhishwa na maendeleo ya ujenzi wa meli mpya ya MV. Mwanza Hapa Kazi Tu wenye thamani ya Shilingi Billion 109 na ikikamilika ndio itakuwa meli kubwa katika Ukanda wote wa Ziwa Victoria na hivyo kuipongeza Kampuni ya Huduma za Meli (MSCL) kwa usimamizi mzuri unaofanywa.

"Kukamilika kwa kwa ujenzi wa meli hiyo kutasaidia sana kuongeza wigo wa shughuli za kiuchumi na mapato mbalimbali yatakayopatikana kwa Serikali ya Tanzania," Bi Sauda alisema.

Bi. Sauda aliyasema hayo baada ya Bodi hiyo iliyoambatana na menejimenti ya BOT Tawi la Mwanza kutembelea mradi huo tarehe 27 Aprili, 2023.

Aidha Bodi hiyo iliwahimiza Menejiment ya MSCL kujitahidi kusimamia mradi huo ili uweze kukamilika kwa wakati na watanzania waweze kunufaika na uwekezaji huo uliofanywa na Serikali.

Kwa niaba ya Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya MSCL Prof. Costa Ricky Mahalu ameishukuru Bodi ya Wakurungezi BOT kwa kufika kwenye mradi huo na kujionea uhalisia wa pesa zilizowekezwa na Serikali ya awamu ya sita katika kuboresha miundombinu ya sekta ya usafirishaji kwa njia ya maji

Mradi wa ujenzi wa Meli ya MV.Mwanza Hapa Kazi Tu, unatarajiwa kukamilika mwishoni wa mwaka huu 2023. Meli hiyo itakuwa na uwezo wa kubeba abiria 1,200 na tani 400 za mizigo pamoja na magari madogo 20 na malori 3.

Naibu Gavana uthibiti na usimamizi wa sekta ya fedha wa Benki ya Tanzania (BOT) Bi. Sauda Kassim Msemo akiongea kwa niaba ya Mwenyekiti wa Bodi mara baada ya kutembelea mradi wa MV. Mwanza Hapa Kazi Tu.

MSCL YAWATUNUKU WATUMISHI 11 MEI MOSI

Na. Kelvin Mmanda

Katika kusherehekea Siku ya Wafanyakazi Duniani maarufu kama Mei Mosi, Kampuni ya Huduma za Meli (MSCL) imewatunuku watumishi wake 11 vyeti na vikiambatana na zawadi kwa utumishi bora katika sherehe hizo zilizofanyika kimkoa katika kata ya Nyampulukano, Wilaya ya Sengerema, Mkoani Mwanza.

Akizungumza baada ya kukabidhi vyeti kwa watumishi hao Mwenyekiti wa Chama cha Wafanyakazi wa Shughuli za Meli na Bandari Tanzania (DOWUTA) Tawi la Mwanza Ndg. Mohamed Rume amesema kuwa watumishi hao wanastahiki kupatiwa zawadi kwa utendaji wao jambo ambalo litawapa moyo wa kuongeza bidii ya kazi katika kutekeleza majukumu yao.

"Tunaishukuru MSCL kwa kuendelea kutoa zawadi na vyeti kwa wafanyakazi wanaofanya vizuri, hii ni haki yao, wanaofanya vizuri wanatakiwa kupewa motisha ili wafanye vizuri zaidi na wengine waone wivu na wao washindane katika kutoa huduma bora ili watunukiwe,"

"Tunaishukuru MSCL kwa kuendelea kutoa zawadi na vyeti kwa wafanyakazi wanaofanya vizuri, hii ni haki yao, wanaofanya vizuri wanatakiwa kupewa motisha ili wafanye vizuri zaidi na wengine waone wivu na wao washindane katika kutoa huduma bora ili watunukiwe," Alisema.

Akiongea wakati wa sherehe hizo Mratibu wa Shirikisho la Vyama huru vya wafanyakazi Tanzania (TUCTA) Mwanza Ndg. Zebedayo Athumani amesema kuwa baadhi ya waajiri wanakiuka sheria, hawawasilishi michango ya watumishi kwenye mifuko ya jamii, hawatoi mikataba ya ajira na hawalipi mishahara kwa wakati.

Katika hotuba yake Mkuu wa Mkoa wa Mwanza Mhe. Adam Malima alisema kuwa Serikali ya Awamu ya Sita inazidi kujali maslahi ya watumishi wa serikali kwa kuwalipa kiasi cha Shilingi Bilioni 1.74 kwa watumishi 571 walioghushi vyeti na Shilingi 660 walilipwa watumishi 503 za Malimbikizo yasiyo ya mshahara.

Siku hiyo ya Wafanyakazi Duniani 2023 iliendeshwa na Kauli Mbiu isemayo "Mshahara bora na ajira za staha ni nguzo kwa maendeleo ya wafanyakazi" na kuhudhuriwa na viongozi mbalimbali wakiongozwa na Mkuu wa Mkoa Mhe Adam Malima kama Mgeni rasmi wa sherehe hizo.

Waliotunukiwa zawadi ya watumishi Hodari ni Deodatha Charles Kweyunga, Bakari Said Kibinda, Zena Ramadhani Mbahe, Kizito Leonard Mugyabuso, Evarist Maganga, Abdulrahman Salim Ally, Japhet Antipas Shirima, Kariuki David Njenga, Lupakisyo Augustino Mwakubali, Novatus Alphonce Kisusi, na Raphael Hitler Nkulamasala.

Baadhi ya watumishi wa Kampuni ya Huduma za Meli (MSCL) na wanachama wa Chama cha Wafanyakazi wa Shughuli za Meli na Bandari Tanzania (DOWUTA) wakiwa kwenye maandamano ya sherehe ya siku ya wafanyakazi Duniani, Mei Mosi mwaka huu.

WAJUMBE WA BODI YA MSCL WAPATA SOMO ZIWA NYASA

Na Shani Chogero

Bodi ya Wakurugenzi ya Kampuni ya Huduma za Meli (MSCL) ikiongozwa na Kaimu Mwenyekiti wa Bodi hiyo Balozi Prof. Costa Ricky Mahalu amesema amejifunza mengi baada ya kufika katika Bandari za Itungi na Kiwira zilizopo Wilayani Kyela, Mkoani Mbeya na kujionea shughuli mbalimbali zinazofanywa na MSCL Tawi la Kyela.

Wajumbe hao wamefanya ziara hiyo kwa lengo la kujifunza na kuweza kuisimamia MSCL katika utekelezaji wa malengo ya Serikali yenye dhamira ya kuboresha Sekta ya Usafiri na usafirishaji wa abiria na mizigo kwa njia ya maji kwenye maziwa makuu nchini.

Akizungumza kwa niaba ya Mwenyekiti wa Bodi hiyo Balozi. Prof. Costa Ricky Mahalu alisema kuwa dhamira ya kufika kwenye bandari hizo ni kujifunza na kushuhudia shughuli zinazofanywa na MSCL na hatimaye kujiweka tayari kwa ajili ya kuzisimamia kwa ufanisi ili kuleta tija kwa mapato ya Serikali na kuboresha huduma kwa wananchi.

"Lengo la kuja huku ni kwa ajili ya 'Orientation' (kufahamu mwelekeo) ili wajumbe wa bodi waweze kufahamu shughuli hizi za MSCL zinakwenda mpaka wapi, kwahiyo kama zilivyo Ziwa Victoria na Tanganyika na leo tupo Ziwa Nyasa, pia tumekuja kuziona hizi meli ambazo kwa muda mrefu zimekuwa zikimilikiwa na Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari (TPA) na miundombinu mengine ambayo MSCL inaweza kupewa kutoka TPA", Alisema.

Tawi la MSCL Kyela lina Meli 5; MV Mbeya II inayobeba abiria 200 na tani 200 za mizigo, MV Njombe na MV Ruvuma zinayobeba tani 1,000 za mizigo, MV Songea inabeba abiria 212 na tani 50 za mizigo na MV Iringa inabeba abiria 139 na tani 5 za mizigo.

Wajumbe wa Bodi ya Wakurugenzi ya MSCL Balozi. Prof. Costa Ricky Mahalu (wa tatu toka kushoto) na Nahodha Ibrahim Bendera (wanne toka kushoto) wakimsikiliza Mkurugenzi wa Huduma za Meli na Utaratibu wa Shughuli za Bandari TPA Nahodha Yusuph Mwingamno ambaye pia ni Mjumbe wa Bodi ya MSCL mara baada ya Bodi hiyo kutembelea meli zilizokuwa chini ya TPA katika bandari ya Itungi, Wilayani Kyela.

MKURUGENZI MSCL ATOA SHUKRANI KWA WADAU BURUNDI NA DRC

Na Shani Chogero

Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya Huduma za Meli (MSCL) Ndg. Eric Hamissi amewashukuru wadau wa sekta ya uchukuzi kutoka nchi ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Watu wa Kongo (DRC) pamoja na Jamhuri ya Burundi kwa kutoa maoni yenye mtazamo wa kuimarisha miundombinu ya usafiri kwa njia ya maji kwa nchi za Afrika Mashariki inayolenga kuinua uchumi wa nchi hizo.

"Tunawashukuru sana kwa ushirikiano wenu, kwa sababu tunaona kabisa kuwa ninyi ni wenzetu kwenye biashara, ni marafiki zetu na tunaona kabisa kuwa tunaweza kufanya biashara kwa hiyo katika hili pia naomba Mheshimiwa Balozi utufikishie salamu zetu kwa Serikali kwamba tunafanya biashara vizuri na hii jumuiya ya wafanyabiashara ya watu wa Burundi," Alisema.

Ametoa shukrani hizo tarehe 30.06.2023 wakati mkutano maalum wa kupokea maoni ya taarifa ya utafiti wa awali uliofanyika katika nchi hizo uliolenga kutambua gharama za usafiri na usafirishaji wa abiria na mizigo katika Ziwa Tanganyika, taarifa iliyowasilishwa na timu ya utafiti wa kimasoko ya MSCL iliyoongozwa na Mkuu wa Kitengo cha masoko na Uhusiano kwa Umma Ndg. Anselm Namala.

Aidha kwa upande wake Kaimu Balozi wa Tanzania nchini Burundi Mhe. Joachim Nyingo aliwasisitiza wadau hao kuendeleza mshikamano wa nchi za Afrika Mashariki na kuhakisha wanaendeleza ushirikiano kwa maendeleo ya wananchi wa nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) pamoja na nchi za Soko la Pamoja la Mashariki na Kusini mwa Afrika (COMESA).

"Burundi ni Mwanachama wa COMESA, ni mmojawapo kati ya nchi 21 za COMESA na Makamu Mwenyekiti wa COMESA ni Mburundi na mwakani Mkutano wa Marais wa COMESA utafanyika hapa, Bujumbura, Burundi umezifikia nchi 21 za COMESA kwahiyo hilo nalo tuwe nalo," Alifafanua.

Mkutano huo umefanyika katika ukumbi mdogo wa Ubalozi wa nchi ya Tanzania nchini Burundi na kuhudhuriwa na wadau wa taasisi 12 kutoka DR Congo na Burundi.

Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya Huduma za Meli (MSCL) Ndg. Eric Hamissi akiongea na wadau wa Sekta ya Uchukuzi katika mkutano uliofanyika katika ukumbi mdogo wa Balozi wa Tanzania nchini Burundi wakati wa ziara ya utafiti wa kimasoko katika mchi zinazolizunguka Ziwa Tanganyika

SHUKRANI ZA KIPEKEE KWA KUFANIKISHA JARIDA HILI

BODI YA WAHARIRI

MWENYEKITI - ERIC B. HAMISSI
MHARIRI MKUU - ANSELM NAMALA
MHARIRI MSAIDIZI - ABDULRAHMAN SALIM

WAJUMBE

EUGENIA PUNJILA
ANTHONY STEPHEN
BARAKA BIGAMBO

BANDARI YA MWANZA KASKAZINI,
JENGO LA TPA, SAKAFU YA PILI
S. L. P. 2385, MWANZA,
Hotline: +255 739 606 600
Barua Pepe: info@mscl.co.tz
Tovuti: www.mscl.co.tz

HALIUZWI

JARIDA HILI IMEANDALIWA NA KUTOLEWA NA KAMPUNI YA HUDUMA ZA MELI